

DIRA YA MAENDELEO TANZANIA 2025

- ✓ Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania wote
- ✓ Kujenga utawala bora na kuzingatia Sheria
- ✓ Kujenga uchumi imara na thabiti unaoweza kukabiliana na ushindani wa Kimataifa.

MPANGO WA TATU WA MAENDELEO YA TAIFA WA MIAKA MITANO (FYDP III)

Kuboresha miundombinu na huduma za TEHAMA na kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwenye viwanda.

SERA YA TAIFA YA TEHAMA

Kujenga, kusambaza na kutumia TEHAMA, ili kuiwezesha jamii ya Kitanzania kuwa na maarifa kupitia matumizi ya TEHAMA.

ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA TAWALA

Umuhimu wa miundombinu ya mawasiliano katika kujenga, kufanikisha na kudumisha uchumi endelevu, kuinua ubora wa maisha na kuimarisha viwango vya maisha ya Watanzania.

MASUALA MUHIMU

- ✓ Kupatikana kwa huduma za Mawasiliano zilizo nafuu katika maeneo yasiyo na huduma hizo au ambayo yamefikishiwa huduma hizo lakini ni duni;
- ✓ Usimamizi wa rasilimali za mawasiliano
- ✓ Matukio ya uvunjifu wa usalama mtandaoni na matumizi mabaya ya mitandao;
- ✓ Upatikanaji wa uhakika wa huduma za mawasiliano na zenye ufanisi;
- ✓ Huduma za Utangazaji zilizo imara na thabiti;
- ✓ Utekelezaji na uendeshaji wa Mradi wa Taka za Kielektroniki;
- ✓ Kufuatilia ubora wa miundombinu na huduma za mawasiliano;
- ✓ Ukuzaji wa uvumbuzi katika sekta ya mawasiliano ili kuharakisha ukuaji wa uchumi wa kidijiti;
- ✓ Uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo na viwango;
- ✓ Uelimishaji wa umma katika masuala ya kidijitali na uelewa wa watumiaji kuhusu huduma za mawasiliano;
- ✓ Ujenzi na uendelezaji wa mifumo ya kutoa huduma na usimamizi wa sekta ya mawasiliano ;
- ✓ Utafiti na durusi kuhusu huduma zinazosimamiwa pamoja na teknolojia mpya za TEHAMA;
- ✓ Kushirikisha wadau na kushirikiana nao katika kusimamia sekta ya mawasiliano.

DIRA

Jamii inayowezeshwa na huduma za mawasiliano.

DHIMA

Kusimamia huduma za mawasiliano kwa ustawi wa jamii ya Kitanzania.

MALENGO YA KIMKAKATI

- ✓ Kukuza miundombinu ya mawasiliano na yenye ufanisi, uhakika na salama imara pamoja na matumizi yake.
- ✓ Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu.
- ✓ Kuimarisha uvumbuzi kwenye huduma za mawasiliano pamoja na uzalishaji na uhifadhi wa maudhui ya ndani katika huduma zinazosimamiwa.
- ✓ Kuimarisha utendaji na ufanisi wa huduma zinazosimamiwa na ulinzi wa wadau.
- ✓ Kuimarisha uwezo wa Kitaasisi.

MATOKEO YA MKAKATI

- ✓ Kupatikana kwa huduma za mawasiliano zilizo za uhakika na salama ;
- ✓ Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu ;
- ✓ Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
- ✓ Kukua kwa ufanisi wa sekta ya mawasiliano na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo, kanuni ndogo na viwango kwa wadau wa sekta ya mawasiliano ;
- ✓ Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.

LENGO LA MAENDELEO

Kuimarika kwa huduma za mawasiliano zinazopatikana kwa wote na kwa bei nafuu.

